SALAMU ZA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA SHEREHE ZA MEI MOSI, 2017 ZILIZOTOLEWA NA MHE. SAIDI M. SADIKI, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO TAREHE 01/05/2017

- Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Mhe. Samia Suluhu Hassan – Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) – Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu);
- Ndugu Tumaini Nyamhokya – Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);
- Ndugu Dkt. Yahaya Msigwa – Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);

- Waheshimiwa Mawaziri , Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara;
- Ndugu Mary Kawar – Mwakilishi wa ILO;
- Ndugu Almasi Maige – Rais wa Chama cha Waajiri;
- Waheshimiwa Mabalozi;
- Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi;
- Viongozi Waandamizi wa Serikali;
- Ndugu Wananchi na Wafanyakazi wenzangu;
- Waandishi wa Habari;
- Wageni Waalikwa;
- Mabibi na Mabwana:

Mheshimiwa Rais;

Napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kukubali mwaliko wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUCTA) kuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha sherehe hizi muhimu sana za wafanyakazi na hasa tukizingatia kuwa unayo majukumu mengi sana ya Kitaifa na Kimataifa.

Aidha, napenda pia kukukaribisha katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro. **Tunakukaribisha sana, jisikie uko nyumbani.** Tunajisikia pia raha na furaha kubwa kuwepo kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ukiondoa Mkoa wa Dar es Salaam na sasa Dodoma, sina kumbukumbu ni mwaka gani ambapo sherehe za Mei Mosi Kitaifa ziliwahi kufanyika Kitaifa Mikoani na viongozi Wakuu wa Kitaifa wote wakawepo. Hii ni heshima kubwa mliyotupa wana-Kilimanjaro na haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Rais;

Tunakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya ya kutuongoza sisi Watanzania. Tuna imani kubwa nawe kupita kiasi. Aidha, sisi wana-Kilimanjaro pamoja na wafanyakazi wote tumepata heshima kubwa kuwa nasi leo hii pamoja na kuwa unayo majukumu mengi Kitaifa na Kimataifa. **Tunakushukuru sana!**

Aidha, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya wana-Kilimanjaro kuipongeza Serikali yako ya awamu ya tano kwa kazi nzuri ambayo imefanywa katika Mkoa wetu tangu ulipoingia madarakani na Wasaidizi wako Wakuu Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwetu sisi wana-Kilimanjaro umetufanyia mambo mengi sana katika muda mfupi wa uongozi wako. Naomba nitaje machache.

(i)Katika kutekeleza utoaji wa elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne, Mkoa umepokea shilingi bilioni **18.292.** (Shule za sekondari shilingi bilioni **13.144** na shule za msingi shilingi bilioni **5.147).** Hali hii imesaidia sana Mkoa wa Kilimanjaro kuendelea kuwa na idadi nzuri ya wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la awali, la kwanza na kidato cha kwanza.

(ii) Agizo lako la watoto wote Shuleni kukaa kwenye madawati limetia hamasa na sasa wanafunzi wote wa Shule za Msingi na Sekondari wanakaa kwenye madawati na tuna ziada ya madawati (**11,978** Shule za Msingi) na (**4,710** Shule za Sekondari).

- Aidha, Serikali imetupatia shilingi milioni **71,161,200/=** kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana kwa shule ya sekondari Oshara na ujenzi umeshaanza. Shilingi **2,083,981,564/=** kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi na shilingi 259,000,000/= kwa ajili ya ujenzi na Maabara katika shule ya sekondari Kamwala iliyoko Wilaya ya Mwanga.

(iii) Kwa upande wa barabara, nafarijika kukuarifu kuwa, Serikali imeshatoa fedha shilingi bilioni **52** kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kilometa **32.2**

kutoka Sanya Juu mpaka Elerai. Kwa sasa Mkandarasi ameshaanza kazi na kutokana na mradi huo, Watanzania wapatao **320** wamepata ajira. Aidha, Mkandarasi anatarajia kukamilisha kazi hiyo ifikapo mwezi **Oktoba, 2018.**

Mheshimiwa Rais; napenda pia kuipongeza Serikali kwa kuweza kutupatia fedha kupitia World Bank kiasi cha shilingi bilioni **13.210** kwa ajili ya ujenzi wa barabara km. **10.67** kwa kiwango cha lami katika Manispaa yetu ya Moshi. Hadi sasa ujenzi wa km. **7.05** umeshakamilika na kazi inaendelea kwa kasi na inatarajiwa kazi itakamilika ifikapo mwezi Agosti, 2017.

Aidha, katika kuboresha barabara za Manispaa ya Moshi kwa kiwango cha lami, Serikali ilitenga shilingi bilioni **4.074** kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi na muda maalumu km. **14.044.**

Hadi sasa Serikali imeshatoa shilingi bilioni **2.734** na matengenezo ya km. **6.38** yameshakamilika na kazi inaendelea.

(iv) Kwa upande wa afya, tunao mradi wa ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto katika Hospitali yetu ya Mkoa ya Rufaa, Mawenzi. Serikali imeshatupatia shilingi milioni **800** na kazi ya ujenzi inaendelea na bado tunatarajia kuwa Serikali itatupatia shilingi bilioni **8** ili kuweza kumalizia ujenzi wa Wodi hiyo na hatimaye kuanza kutumika. Ujenzi wa Wodi hiyo ya ghorofa 3 ulioanza mwaka 2009 ulisimama kwa miaka minne (4) unaendelea kwa kasi ndogo kulingana na fedha kidogo zinazotolewa. Kazi ya ujenzi na usimamizi inafanywa na Wakala wa Majengo (TBA).

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Siha: Serikali imetupatia shilingi milioni **250** na ujenzi unaendelea vizuri.

(v) **Mheshimiwa Rais;** tunakupongeza kwa agizo lako la kuelekeza Walimu na Madaktari waajiriwe. Katika Mkoa wetu tumepangiwa Walimu **100** wa masomo ya Sayansi na tayari Walimu **94** wamesharipoti na kupangiwa kazi.

Aidha, agizo lako la kuajiri Madaktari **258** hapa nchini tumepokea kwa shangwe kubwa na tuna imani kubwa kuwa Mkoa wetu utakuwa ni kati ya Mikoa itakayopangiwa Madaktari hao. Hatua hii itasaidia sana kupunguza tatizo la upungufu wa Madaktari katika vituo vya kutolea huduma.

Mheshimiwa Rais; ni vyema pia nikatumia fursa hii kukupongeza kwa maelekezo yako ya kuhakikisha dawa zinapatikana katika Hospitali zetu. Mwaka **2015/2016** Mkoa ulipokea shilingi bilioni **3.7** na mwaka huu hadi Aprili, 2017 tumeshapokea shilingi bilioni **6.0** ikiwa ni

ongezeko la zaidi ya asilimia **100** ukilinganisha na fedha tulizopokea mwaka wa fedha uliopita. Kwa hali hiyo, hivi sasa katika Mkoa wetu dawa zinapatikana vizuri katika vituo vyote vya kutolea huduma na dawa hizo zinasambazwa moja kwa moja na Bohari ya Dawa (MSD) kwenda katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Rais; kazi kubwa imefanyika ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Upatikanaji kwa Vijijini ni asilimia **79** na Mijini ni asilimia **98.** Aidha, kwa sasa Mkoa una mradi mkubwa wa Kitaifa wa Mwanga, Same, Korogwe utakaogharimu shilingi **41,356,702.15** (awamu ya kwanza) ambao umeshaanza kutekelezwa na Serikali inachangia asilimia **50** ya gharama za mradi huo, BADEA asilimia **20** na OFID asilimia **30.** Hadi sasa awamu ya kwanza ya mradi umekamilimia kwa asilimia **19.4.** Mradi huu unararajiwa kukamilika mwezi Julai, 2017 lakini uko nyuma ya wakati kwa ukosefu wa fedha huko nyuma.

Lakini kutokana na umahiri wako wa kutafuta fedha na kuzigawa fedha hizo, mradi huu umeanza kuendelezwa kwa kasi kubwa baada ya Mkandarasi M/S Kharal kulipwa malipo yake aliyokuwa anaidia Serikali.

Mheshimiwa Rais;

Napenda kukuarifu kuwa, katika Mkoa wetu wafanyakazi wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingitia kanuni, taratibu na sheria. Aidha, Mkoa umeendelea kusimamia hili na pale kunapokuwa na utendaji usioridhisha waajiri wameendelea kuwachukulia hatua wafanyakazi kupitia mamlaka zao za nidhamu.

Mheshimiwa Rais;

Kama zinavyoelekeza sheria, kanuni na taratibu za kazi katika nchi yetu, Serikali ya Mkoa imekuwa ikisisitiza na kusimamia uanzishwaji wa matawi ya Vyama vya

Wafanyakazi pamoja na uwepo wa Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi.

Napenda kukufahamisha kuwa uwepo wa utaratibu huu umekuwa na tija sana kwa wafanyakazi na waajiri na hivyo kupelekea kuwa na utendaji kazi mzuri na hali ya usalama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Rais;

Nafahamu kuwa wananchi/wafanyakazi wanayo hamu kubwa ya kukusikiliza.

Naomba kwa mara nyingine tena kukukaribisha Mkoani Kilimanjaro.

MSHIKAMANO!!

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!